KABLA ya kufunga mwaka wa 1982, Rais Daniel Arap Moi amakuwa na shughuli nyingi za kitaifa na Kijamii katika pembe tofauti za Jamhuri ya Kenya. Akiwa Nairobi, Kabarak, Kisii, Nyeri, Muranga, ameweza katika sehemu zote hizi kushuhudia matukio mbali mbali, kuhutubia wananchi waliomtembelea, kukagua shughuli za maendelo, kuhudhuria tafrija mbali mbali na kujumuika na Wakenya wote katika sherehe za Krismas. Rais Moi aliweza tena kudhihirisha upendo wake kwa wananchi, na kuwaongoza katika falsafa ya Nyayo inayohimiza Upendo, Amani na Umoja kwa Wakenya wote nchini.



*RAIS MOI akiondoka baada ya kutembelea kituo cha Kenya Pipeline Company, Nairobi, kilichoshika moto wiki jana.*



*RAIS MOI anaonekana akizungumza na wauguzi wa hospitali ya Nyeri alipotembelea hospitali hiyo.*



*RAIS MOI akikagua miche ya chai katika shambo moja huko Muranga akiwa njiani kutoka Nyeri.*



*MTUKUFU RAIS MOI akipeana zawadi kwa Bi. Angela Nyachae bintiye katibu wa kudumu katika Afisi ya Rais Bw. Simon Nyachae pamoja na Bw. Joseph Mageto katika harusi yao iliyofanyika katika kanisa la Kisii.*



MCHA MUNGU — *Rais Moi akihudhuria ibada ya kanisa wakati wa Krismas kwenye kanisa la African Inland Church, Nakuru.*

PICHA ZOTE — KENYA NEWS AGENCY

# ATHARI YA MARUNGI KWA WAISLAMU

NA ZUBEIR NOOR

**KATIKA wiki chache zilizo pita kupitia katika gazeti hili hili nilieleza ubaya na uchafu unaotokana na kuweko kwa magar den katika mitaa yetu ya Mombasa na nikagusia juu ya uvutaji wa bangi na ulaji wa marungi.**

**Leo nitaeleza kinaganaga juu ya Athari na hasara kubwa inayowapata jamii ya kiislamu katika Kenya na hasa hapa pwani ndio zaidi. Nikitilia mkazo zaidi ubaya wa marungi ama waeza kusema GHAAT, GIZA N.K.**

**Kama miaka 30 iliyopita marungi yalikuwa yakitafunwa na waarabu wa makamo wakati wa Jumamosi na Jumapili, hasa zaidi katika sherehe za harusi wakiwa wanatumbuizwa kwa nyimbo na muziki wa taarabu. Haya marungi kulingana na hao jamaa yalikuwa yakiwafanya wawe macho usiku kucha huku wakipiga makofi na kustarehe.**

**Kwa hakika ulaji huo na sherehe miaka hiyo iliyopita ilikuwa ikianza baada ya swala za Isha hadi saa saba za usiku na sio asubuhi kama ilivyo sasa. Hufanywa hivi ili watu wa wahi kupata kuswali swala ya asubuhi.**

**Kwa hivyo wakati huo walaji wa marungi walikuwa hawaathiriwi sana kimwili wala walikuwa hawakosi kumwabudu MWENYEZI MUNGU.**

**Hata hivyo kila kukicha mambo yalizidi kubadilika. Miaka kumi iliyopita ulaji wa marungi ulikubaliwa kuliwa hadharani bila ya pingamizi yeyote kutoka kwa wale tunaowapa kura na kuwachaguwa wawe macho yetu mbele ya bunge na serikali.**

**Kwa vile wengi wao ni walaji bora wa marungi na masaa yao mengi hutumia kwa kula marungi na usistaajabu kuona ndugu hawa wale washauri wao na wasaidizi wao ni mabingwa wa kula marungi.**

**Sasa kuanzia hapo ndugu zetu waislamu wa Pwani badala ya wao kununua na kula marungi bali walbadilika kuwa wauzaji na naajenti wa kutafuta walaji marungi. Wengine walitowa na kununua magari na kujenga vibanda kila mahali vya kubeba na kuuza marungi.**

**Mambo sasa ndio yakawa mabaya zaidi kwa sababu hapo mbeleni watu walikuwa wakiabudu Mwenyezi Mungu, sasa imekuwa kuabudu ulaji wa marungi. Hata kuswali imekuwa ni dhambi. Kwa sababu hawana wakati huo wa kuswali ikiwa mtu anaanza kula marungi kutoka asubuhi.**

**Zaidi athari ya kula marungi asubuhi na mchana im leta hasara kubwa kwa jamaa hawa kimwili. Magonjwa yasiyo juli kana kichwa wala maguu.**

**Imefika wakati ambapo ulaji wa marungi na waislamu umezidi na kupita kiasi na hivi sasa hasari kubwa iliyopa ikiwa ni ya kusikitisha sana kupita mpaka.**

## KAMA MBUZI

**Jambo moja la ajabu ni kwamba walaji hawa wa marungi wamewashinda hata wanyama kama mbuzi, ambao nao wanaongoza katika utafunaji wa majani ulimwenguni. Wengine hulala na huku wakiwa na wasiwasi kama atapata pesa za kununua marungi.**

**Mtu huyo hawezi kunywa hata chai ya asubuhi hadi usiku wa manani ikiwa mfuko wake ni mnono. Kama hana atakopa, au aibe lakini lazima ale marungi. Kama vile ni chakula bora kinachohitajika sana katika kujenga na kulinda mwili wake**

## SWAHIBU

**Mtu huyo aweza kuwa ni baba ama mzee wa nyumba amapengine ni babu hapo kwake nyumbani. Kwa ajili ya nakhwa na ulevi wa marungi amekuwa hajali wala hana haja ya mke wake, wanawe ama wajukuu wake. Rafiki yake na swahibu wake mkubwa sasa ni marungi.**

**[ITAENDELEA]**



*MBUNGE Juma Boy ambaye ni Katibu wa COTU akipeana zawadi na hati za utumishi kwa wafanyakazi wa East African Industries kwenye karamu yao ya Krismasi, Nairobi.* PICHA: KENYA NEWS AGENCY



*PICHANI ni vijana kutoka shule ya Shimo-La-Tewa Tudor walioshiriki katika "President's Award Scheme " huko katika milima ya Taita.*



PICHA: NATIONAL STUDIO

*MTUMISHI hodari T. Mukwana (pichani) akivishwa beji ya heshima kwa utumishi wake wa miaka 25 na meneja mkuu wa Kenya Shell Company Bw. N.J. Muriuki kwenye tafrija ilifofanywa hapa Mombasa wakati meneja wa Mombasa Bw. Luckett akitazama.*




*BW. ALI MBARAKA akipokea zawadi yake ya television ya rangi kutako kwa meneja wa Coastal Bottlers Bw. M. Qoyyan baada ya kushinda katika mashindano ya Maendeleo ya Wanawake yaliyodhaminiwa na Coca-Cola Africa Limited.* PICHA: NATIONAL STUDIO

# JISHINDIE

## MIAVULI AU T-SHIRT MARIDADI KATIKA SHINDANO JIPYA LA KUJAZA MANENO

*KWENDA KULIA:*

1. United Kingdom
3. Moyo
8. Sehemu ya mnyama
10. Nchi Arabuni
11. Langalie
12. Mahali penye maji mengi baharini
13. Nguvu za Mungu
18. Wazimu
21. Hutengeza bara bara
23. Uadilifu
24. Natasi, sehemu ya ardhi
25. Zuia vita
26. Atatunga ndoa
27. Tamko la kukataa.

*KWENDA CHINI:*

1. Ukoa haigeuki
2. Mtoto wa ndege
4. Uchatu
5. Sikukuu ya Kiislamu
6. Silaha za kutatunia
7. Sikwamba hana
8. Mwiko zaidi ya mmoja
9. Aeu kama ilivyo
14. Bembeleza
15. Shirika, Mkao
16. Wenyeji wa nchi
17. Taka kitu kimombo
18. Cha kujiangalia
19. Kiungo cha maneno
20. Azidi kimo
21. Tunza mtoto
22. Ota, chipuza.

**Washindi wa Fumbo la Kujaza Maneno No. 152**

1. Ali Bakari Sanduku La Posta 86922 Mombasa.
2. P. W. Mpwipniro Sanduku la Posta 90404 Mombasa.
3. Jimmie Munene Sanduku La Posta 87310 Mombasa.

**Washindi waombwa wafike afisini mwa** *COASTWEEK*.


**MAJIBU YA SHINDANO LA FUMBO LA KUJAZA MANENO NO 152 —**

*KWENDA KULIA:*

1. KUNGU, 6. KAZA, 7. NAAM, 10. ADAI, 11. ANAO, 12. SH, 13. BA, 14. HIMU, 16. TAIB, 18. JA, 19. OA, 20. TUMA, 23. BOSS, 25. AZOA, 26. ISHA, 27. UBALE.

*KWENDA CHINI:*

1. KADHI, 2. UZA, 3. NAIBU, 4. UNA, 5. KAA, 6. KASHATA, 8. ANGA, 9. MOMBASA, 15. MUMO, 16. TABIA, 17. IOSHE, 21. UZI, 22. AAU, 24. OSL.




SWAHILI CROSSWORD NO 153

**JINA** ..........................................

**SANDUKU LA POSTA** ..........................................

..........................................

**Shindano la Fumbo la Kujaza Maneno:**

Uamuzi wa majaji utakuwa wa mwisho. Hakuna malamiko yoyote yatakayokubaliwa. Washindi watatu kila baada yawiki mbili watapata miavuli au T-Shirt maridadi. Shindano hili limeshaminiwa na *COASTWEEK* Limited Mombasa., Jawabu za Fimbo hili lipelekwe kwa: *Muhariri COASTWEEK, Sanduku La Posta 87270 Mombasa, Kenya.* Siku ya Jumatano tarehe **January 5, 1983.** saa nne asubuhi shindano hili litakuwa mwisho.